



WAKALA WA USAJILI UFILISI NA UDHAMINI



(RITA)

TAARIFA KWA UMMA

**KUONGEZWA KWA MUDA WA UHAKIKI WA VYETI VYA
KUZALIWA NA VIFO KWA WANAFUNZI WANA OOMBA
MIKOPO YA MASOMO YA ELIMU YA JUU
MWAKA 2017/2018**

Tunapenda kuufahamisha umma kwamba muda wa kupokea maombi ya uhakiki wa vyeti vya kuzaliwa na vifo umeongezwa hadi tarehe 07 Septemba 2017.

Hivyo tunatoa wito kwa waombaji wote wa Mikopo ya Masomo ya Elimu ya juu ambao bado hawajawasilisha vyeti vyao kwa ajili ya kuhakikiwa wahakikishe wanatuma maombi ndani ya muda huo. Baada ya tarehe hiyo ,Ofisi itashughulikia maombi yaliyotumwa kwa njia ya barua pepe au kuwasilishwa moja kwa moja katika Ofisi zetu zilizopo kwa Wakuu wa Wilaya na RITA Makao Makuu na kutoa majibu kwa waombaji.

Aidha wananchi waliotuma maombi yao kwa njia ya barua pepe wanaendelea kujibiwa na wale ambao waliwasilisha katika Ofisi yetu ya Makao Makuu Jijini Dar es salaam wanaweza kufika siku ya jumamosi ya tarehe 02 Septemba 2017 kwani huduma ya uhakiki itaendelea kutolewa kama kawaida.

Emmy Kalomba Hudson
Kaimu Afisa Mtendaji Mkuu – RITA
31 Agosti 2017